**Issue no:** 01 | **Vol no:** 06 | **August** 2025: 24-34

# Mikakati Inayotumiwa na Viongozi Kukabiliana na Changamoto Zinazokumba Uafikiaji wa Malengo ya Maendeleo Endelevu katika Tamthilia Teule za Kiswahili

**Samuel Sinzore Ogonda**[1]
**Isaac Odeo Ipara**[2]
**Amukowa Deborah**[3]

**Article History**
Received: **2025.06.14**
Accepted: **2025.07.13**
Published: **2025.08.15**

(**1.2**) Kibabii University, Kenya; (**3**) Maseno University, Kenya.
Main author's email: sasio.ogonda@gmail.com

**Cite this article in APA**
Ogonda, S. S., Ipara, I. O., & Amukowa, D. (2025). Mikakati inayotumiwa na viongozi kukabiliana na changamoto zinazokumba uafikiaji wa malengo ya maendeleo endelevu katika tamthilia teule za Kiswahili. *Editon consortium journal of kiswahili, 6*(1). 24-34. https://doi.org/10.51317/ecjkisw.v6i1.615

**Ikisiri**
Lengo la makala hii ni kuchunguza mikakati inayotumiwa na viongozi kukabiliana na changamoto zinazokumba uafikiaji wa MME katika tamthilia teule za Kiswahili. Uongozi ni suala muhimu katika jamii na hudhihirika kupitia mikakati kadhaa, mojawapo ni utekelezaji wa Malengo ya Maendeleo Endelevu (MME). Utekelezaji wa MME unaendelea kukumbwa na changamoto mbalimbali. Utafiti huu ni wa kithamano na uliongozwa na Nadharia ya Uhistoria Mpya iliyoasisiwa na Stephen Greenblatt (1980) na kuendelezwa na Brizee na Tompkins (2012). Muundo wa kiuchanganuzi ulitumiwa. Data ilikusanywa kupitia mbinu ya unukuzi. Data hii ilipangwa kisha kuchanganuliwa kwa njia ya uhakiki wa yaliyomo. Kwa kutumia mbinu ya usampulishaji dhamirifu, tamthilia nne ziliteuliwa. Tamthilia hizi ziliteuliwa kwa msingi kuwa zina maudhui ya uongozi na ziliandikwa kati ya miaka ya 2016 na 2024 ambacho ni kipindi cha utekelezaji wa mpango wa MME. Hizi ni: *Shamba la Halaiki* (Okello, 2016), *Mwinyi na Manyani ya Adili* (Mbogo, 2022), *Kifunganjia* (Okello, 2021) na *Kodi* (Muhando, 2024). Matokeo yamewasilishwa kwa njia ya maelezo ya maandishi. Matokeo ya kazi hii ni kuwa, viongozi wanatumia mikakati mbalimbali kukabiliana na changamoto zinazotatiza uafikiaji wa mpango wa MME. Isitoshe, kushiriki na kuhimiza kilimo ni mkakati ambao unachangia uafikiaji wa malengo kadhaa ya MME. Makala ii inapendekeza kuwa viongozi wawashirikishe raia katika utekelezaji wa mikakati inayolenga kuafikia MME ili maendeleo yaafikiwe kwa pamoja. Aidha, viongozi wa nchi mbalimbali waweke mikakati ambayo itainua sekta ya kilimo kuanzia mashinani kwa kuwa kilimo kitasaidia uafikiaji wa malengo kadhaa ya mpango wa MME.

**Maneno muhimu**: Malengo ya Maendeleo Endelevu (MME), mikakati, tamthilia, uongozi.

Editon OPEN ACCESS

This article is distributed under the license of a Creative Commons Attribution-Non Commercial-ShareAlike 4.0 International License. It is permitted to be used, reproduced and distributed in line with Editon Consortium Publishing guidelines.

## UTANGULIZI

Viongozi hupitia changamoto mbalimbali katika shughuli ya kuwaongoza watu (Njoroge, 2014; Ongarora, 2020). Makala hii iliangazia mikakati inayotumiwa na viongozi kukabiliana na changamoto zinazokumba uafikiaji wa Malengo ya Maendeleo Endelevu (MME) katika tamthilia teule za Kiswahili. Uongozi ni shughuli ya kusimamia na kuelekeza watu au kundi la watu kutekeleza shughuli husika na kuafikia malengo fulani (TUKI, 2014; Dinibutun, 2022). Uongozi ni suala muhimu katika jamii kwa kuwa kiongozi husimamia, huelekeza, huathiri, hushawishi na kuwachochea watu kutekeleza shughuli fulani (Ogonda, 2019). Viongozi wana nafasi muhimu ya kukabiliana na changamoto zinazokumba jamii zao (Ongarora, 2020).

Kwa mujibu wa Mintzberg et al. (2005), mkakati ni mpango au mwelekeo wa jumla wa kufikia lengo fulani kwa kutumia rasilimali zilizopo. Katika kuteleza mkakati fulani, mtu, watu ama shirika hutumia mbinu mbalimbali. Mbinu ni njia mahsusi au namna ya kutekeleza mkakati fulani na hushirikisha mipango ya vitendo vya muda mfupi ambavyo husaidia kufanikisha mkakati (Porter, 1996; Nickols, 2016). MME seti ya malengo kumi na saba yaliyoidhiniswa na nchi zote wanachama wa Umoja wa Mataifa (UM) mwaka 2015 (Gosling-Goidsmith, 2018). Malengo haya yamefumwa pamoja, hufungamana, huhusiana na kutegemeana hivi kwamba ufanisi wa lengo moja huchangia kukamilisha lengo lingine (Griggs et. al, 2017). Mpango huu unalenga kuafikia maendeleo ya kijinsia, usawa wa kimazingira na ukuaji wa kiuchumi (Gossling-Goidsmiths, 2018; Zhai et al., 2023).

Suala la uongozi limeakisiwa katika fasihi na hasa tamthilia tangu jadi ya Wayunani. Katika siku za hivi karibuni, upacha wa mambo haya umejitokeza kwa uzito mkubwa ambapo fasihi haionyeshi tu uongozi kama chombo cha mamlaka, bali pia kama chanzo cha mafanikio au anguko la jamii. Kwa kuangazia suala la uongozi, fasihi kama kioo cha jamii huchangia katika kuafikia maendeleo (Musindalo, 2020). Tamthilia ina nafasi kubwa na muhimu ya kuchangia masuala ya uongozi na maendeleo katika jamii kupitia kwa matendo na maneno ya moja kwa moja ya wahusika (Mulokozi, 1996). Kazi hii ilishughukikia mikakati wanayotumia viongozi kukabiliana na changamoto zinazokumba utekelezaji wa mpango MME. Mjadala wa kina ulikuzwa kurejelea tamthilia teule: *Shamba la Halaiki* (Okello, 2016), *Mwinyi na Manyani ya Adili* (Mbogo, 2022), *Kifunganjia* (Okello, 2021) na *Kodi* (Muhando, 2024) ambazo zilitungwa katika kipindi ambapo MME yanaendelea kutekelezwa (2016-2024). Makala hii ilihusisha sehemu ya utangulizi, mapitio ya maandishi, mbinu za utafiti, matokeo na hatimaye hitimisho na mapendekezo.

## MAPITIO YA MAANDISHI

Sehemu hii ilishughulikia uhakiki wa maandishi kwa kurejelea tafiti za jumla kuhusu uongozi na ukabilianaji wa changamoto katika jamii. Makala hii ni tokeo la tathmini za tafiti mbalimbali zilizoshughulikia maudhui ya uongozi katika fasihi. Kigezo kilichotumiwa katika kuteua tafiti zilizotathminiwa na makala hii ni maudhui ya uongozi hasa kwa kuegemea kwa changamoto zinazowakabili viongozi.

Ntiba (2011) alitafiti kuhusu taathira ya dhamira kwa mtindo katika hadithi fupi teule za Kiswahili. Kwa kuonyesha athari ya kimtindo, alichunguza maudhui kama vile dawa za kulevya, haki za watoto, ugonjwa wa Ukimwi, tamaa ya pesa, migogoro katika ndoa na kutowajibika kwa viongozi wa kisiasa. Kuhusu kutowajibika kwa viongozi wa kisiasa, Ntiba aliibua wazo kuwa viongozi wana jukumu kubwa la kuwaongoza raia ili waweze kupiga hatua kimaendeleo katika nyanja zote za kimaisha. Wazo hili liliwekea utafiti huu msingi wa kuchunguza namna uongozi katika tamthilia teule unavyokabiliana na changamoto zinazozuia uafikiaji wa MME. Ntiba aliegemea taathira ya dhamira kwa mtindo katika hadithi fupi. Kazi hii imejikita katika kuchunguza mikakati inayotumiwa na viongozi kukabilana na changamoto ambazo zinakumba uafikaji wa MME katika tamthilia teule za Kiswahili.

Njoroge (2014) alitafitia viongozi kama visababishi vya mabadiliko katika riwaya mbili za Mwenda Mbatiah: *Vipanya vya Maabara* (2007) na *Majira ya Tufani* (2012). Katika utafiti wake, alibainisha namna mabadiliko yanavyoathiriwa na masuala ya umaskini, ukosefu wa desturi zinazofaa miongoni mwa viongozi na uzembe. Suala la umaskini ni lengo la kwanza (L1) la mpango wa MME. Suala hili lilichunguzwa ili kubaini utekelezaji wake kwa mujibu wa tamthilia teule. Ni kutokana na utekelezaji huu ndipo makala hii iliibua changamoto zinazokabili utekelezaji wa lengo hili na namna viongozi wanasuluhisha changamoto za utekelezaji wake kwa kurejela tamthilia teule za Kiswahili.

Njoroge anawapendekezea watafiti wa baadaye wachanganue namna baadhi ya waandishi wanavyosawiri matatizo katika jamii zao kwa kutumia tanzu mbalimbali za fasihi zikiwemo tamthilia, hadithi fupi na ushairi. Utafiti huu uliangazia matatizo haya ila ukapiga hatua zaidi ya kuangazia namna viongozi wanavyokabiliana na changamoto hizi zinazotishia kudidimiza uafikiaji wa MME. Njoroge alichunguza viongozi kama visababishi vya mabadiliko. Utafiti huu umechunguza uongozi na uafikiaji wa MME. Isitoshe, Njoroge alirejelea utanzu wa riwaya. Amerejelea riwaya mbili: *Vipanya vya Maabara* (2007) na *Majira ya Tufani* (2012) na kubainisha namna viongozi wanavyosababisha mabadiliko katika riwaya hizo. Alitumia nadharia ya Uchanganuzi Hakiki Usemi (NUHU). Makala hii iliongozwa na nadharia ya Uhistoria Mpya. Njoroge alirejelea kazi za fasihi zilizotungwa katika kipindi cha milenia mpya: mwaka wa 2007 na 2012. Kazi hii imerejelea tamthilia za Kiswahili zilizotungwa kuanzia mwaka wa 2016 hadi 2024. Hiki ni kipindi ambapo utekelezaji wa MME unaendelea.

Ogonda (2019) alitafitia taswira ya mwanamke kiongozi katika tamthilia teule za Kiswahili tangia mwaka wa 2000 hadi 2016. Kupitia kwa matendo, mitazamo na mitindo ya lugha iliyotumiwa katika tamthilia alizoziteua, Ogonda alishughulikia baadhi ya changamoto anazokumbana nazo mwanamke katika shughuli ya kuongoza jamii. Baadhi ya changamoto alizozibainisha ni: kudharauliwa, kukejeliwa, kusingiziwa maovu, kupigwa, kutishwa na kutengwa kwa kiongozi wa jinsia ya kike. Changamoto hizi zilisaidia makala hii kuibua changamoto zinazokumba uafikiaji wa MME na hivyo kutambua mikakati inayotumiwa na viongozi kusuluhisha changamoto hizi. Tamthilia zilizorejelewa na Ogonda ni zile zilizotungwa kati ya mwaka wa 2000 hadi 2016. Makala hii iliangazia tamthilia zilizotungwa kati ya 2016 na 2024. Ogonda alijikita katika uongozi wa mwanamke; utafiti huu ulimwangazia kiongozi mwanamke na mwanamume.

Ongarora (2020) alitafitia usasa katika ushairi wa Kithaka wa Mberia kwa kuegemea uchanganuzi wa maudhui na mtindo. Alionyesha namna baadhi ya mashairi ya Kithaka wa Mberia yanavyoangazia changamoto za mataifa ya Afrika. Matatizo haya ni pamoja na vita vya kikabila, mizozo, ukimbizi, njaa, ukosefu wa elimu na uharibifu wa mazingira. Makala hii iliangazia matatizo ya njaa, ukosefu wa elimu na uharibifu wa mazingira kwa kuwa yanahusiana na MME. Kwa kuangazia matatizo haya, utafiti huu ulichunguza namna viongozi wananvyokabiliana na changamoto katika jamii zao. Ni changamoto hizi ndizo zinachelewesha au kudumaza uafikiaji wa MME.

**Nadharia ya Utafiti**

Kazi hii iliongozwa na nadharia ya Uhistoria Mpya iliyoasisiwa na Greenblatt (1980) na kuendelezwa na Brizee na Tompkins (2012). Nadharia hii ina mihimili tatu za msingi. Mhimili wa kwanza ni kuwa masuala ya kifasihi huchunguzwa mintarafu wakati au muhula na mahali. Mhimili wa pili, ni utunzi wa kazi ya fasihi na jamii ambayo kwayo kazi hiyo imeandikwa ni muhimu na wa tatu ni fasihi inaweza kuelezwa nje ya mtungo wenyewe. Mihimili hii miwili ilisaidia kufanikisha kazi hii. Kupitia kwa mihimili hii, vipengele vya utunzi wa fasihi vikiwemo fani na maudhui pamoja na masuala katika jamii ya sasa yametumiwa kubainisha mikakati mbalimbali inayotumiwa na viongozi katika kuendeleza uafikiaji wa MME katika tamthilia teule.

**MBINU ZA UTAFITI**

Utafiti huu ni wa kithamano na ulitumia muundo wa kiuchanganuzi. Kwa mujibu wa Mwanje (2001) mkabala huu ni faafu kwa makala ya kimatini. Muundo huu ulitumiwa kuchanganua masuala ya kiuongozi katika tamthilia teule. Mbinu ya usampulishaji kidhamirifu ilitumiwa kuteua tamthilia nne: *Shamba la Halaiki* (Okello, 2016), *Mwinyi na Manyani ya Adili* (Mbogo, 2022), *Kifunganjia* (Okello, 2021) na *Kodi* (Muhando, 2024). Kigezo kilichotumiwa kuteua tamthilia hizi ni maudhui. Zote zina maudhui ya uongozi. Data ilikusanywa kupitia mbinu ya unukuzi. Tamthilia teule zilisomwa kwa kina na data kuibuliwa kwa usaidizi wa orodha ya uthibitishaji. Data hii ilipangwa kisha kuchanganuliwa kwa njia ya uhakiki wa yaliyomo. Matokeo yaliwasilishwa kwa njia ya maelezo ya maandishi.

Masuala ya kimaadili yamepewa kipaumbele katika kazi hii. Creswell (2003) anaibua hoja kuwa, katika uandishi na usambazaji, mtafiti hafai kudanganya, kuzima au kubatilisha matokeo ya utafiti ili kutimiza mahitaji yake au ya hadhira. Usahihi wa matokeo umezingatiwa kwa kuhakikisha kuwa matokeo hayabatilishwi kwa vyovyote vile. Kila kazi iliyosomwa na kurejelewa katika makala hii imetambuliwa. Haki miliki za watunzi zimezingatiwa kwa kuhakikisha kuwa yaliyoandikwa kwenye vitabu vilivyotumiwa katika utafiti huu hayapunguzwi au kuongezwa. Unukuzi kutoka kwa tamthilia teule umefanywa kwa kurejelea kurasa maalumu na pia bila

kuongeza maneno yoyote ambayo hayapatikani katika tamthilia hizi.

## MATOKEO YA UTAFITI

### Mikakati inayotumiwa na Viongozi Kukabiliana na Changamoto zinazokumba Uafikiaji wa MME

Tafiti mbalimbali kuhusu uongozi katika fasihi zimedhihirisha kwamba uongozi ni suala muhimu katika jamii. Katika karne hii ya 21 viongozi wanapitia changamoto mbalimbali katika azma yao ya kuongoza jamii. Makala hii ilichunguza mikakati mbalimbali inayotumiwa na viongozi katika tamthilia za *Shamba la Halaiki* (2016), *Kifunganjia* (2021), *Mwinyi na Manyani ya Adili* (2022) na *Kodi* (2024) kukabiliana na changamoto ambazo zinakumba utekelezaji wa MME. Mikakati mbalimbali ilibainishwa na kuelezwa ifuatavyo:

### Elimu, Taaluma na Talanta

Mdee et.al (2015) wanaeleza: elimu kama mafunzo yanayotolewa na jamii kwa watu wake, darasani au pasipokuwa darasani; taaluma kama elimu na maarifa yanayopatikana kwa kusoma na talanta kama kipaji alichonacho mtu kinachomwezesha kufanya jambo fulani kwa ufanisi. Katika *Kifunganjia*, Rajua anatumia elimu, taaluma, talanta na ujuzi wake. Amesomea taaluma ya uanahabari hadi kiwango cha uzamili (uk. 87). Anatumia elimu aliyoipata kutafuta suluhu kwa matatizo yanayokumba jamii yake. Mwandishi anatueleza:

> *Rajua, kijana mwenye umri ya miaka takribani ishirini na mitano hivi, anaingia uwanjani. Amebeba kijikamera, kalamu na karatasi. Anasimama karibu na ua wa ghala uliobomolewa. Anaweka kijikamera chake kwenye mhimili mrefu na kukielekeza kwenye ghala (uk. 13).*

Kwa kurejelea muktadha huu, Rajua agunduapo kulikuwa na tatizo la njaa ambalo lilitishia uafikiaji wa L2, anaamua kubomoa ua uliokuwa unazunguka ghala ili watu wajionee hali halisi ya ghala. Kijikamera, kalamu na karatasi ni vifaa muhimu vya taaluma yake ya uanahabari. Anatumia vifaa hivi kuandaa makala ambayo aliyachapisha katika gazeti.

Kando na kutumia elimu na taaluma, Rajua anatumia talanta na ujuzi kuleta mabadiliko katika jamii yake. Anashirikiana na vijana wenzake kama Shari kuigiza kanisani. Anaigiza matendo ya watu fulani katika kitabu kitakatifu ambayo yanaoana na matendo ya watu katika jamii yake . Lengo la maigizo haya ni kuwahamasisha wanajamii kuzinduka na kuleta mabadiliko katika jamii yao (uk. 23). Ujuzi wa Rajua katika uigizaji unabainika katika usemi wa Komba anayemwambia Tembo:

> *Nakwambia kijana huyo! We! Anaigiza kama watu wale niliowaona kwenye runinga ya jirani (uk. 23).*

Kupitia maigizo yake na Mtumishi, kiongozi Rajua anatumia uigizaji kuelezea matatizo yanayowakumba wakulima katika kijiji chake cha Bakunja. Kwa kufanya hivyo, anaendeleza uafikiaji wa L2. Anamwambia Mzee:

> *Kama ujuavyo, nimesomea uanahabari. Ningependa niwe mwanahabari mpekuzi na mwigizaji hodari. Nia yangu kuu ni kutumia elimu na ujuzi wangu kusaka masuluhisho ya masuala mbalimbali kupitia upekuzi na maigizo. Niyaanike peupe kama jua la mchana. (uk.18).*

Kwa maoni ya Ntiba (2011), viongozi wana jukumu kubwa la kuongoza raia ili waweze kupiga hatua kimaendeleo. Kiongozi Rajua anjitolea kuleta maendeleo katika kijiji chake kupitia elimu, taaluma na ujuzi wake.

Unyanyasaji wa kiuchumi katika nchi rejelewa katika tamthilia ya *Kodi* ni tatizo sugu ambalo lilitihia uafikiaji wa L1: Kutokomeza umaskini wa aina yote kila mahali. Mtambaji anatumia jazanda ya jipu kulielezea. Anasema:

> *Mimi mtambaji najiuliza, hivi hasira zote hizi,*
> *jipu hili litapasukia wapi? (uk.102).*

Elimu, talanta na taaluma ni mbinu zinazotumiwa katika tamthilia ya *Kodi* kuhamasisha jamii na kukosoa viongozi kuhusu tatizo la unyanyasaji wa kiuchumi. Uhamasishaji huu unafanyika kupitia taasisi ya elimu. Watoto wanatumia talanta ya sanaa ya ngoma. Waanzilishi wa ngoma hii ni watoto wawili: Shangwe na Mariam ambao wanabuni wimbo huu. Wanatumia ubunifu wao kuleta utatuzi wa changamoto katika jamii ya *Kodi* (uk. 73). Baada ya kubuni wimbo wao, wanaanza kufanya mazoezi ili kujiandaa kwa mashindano siku ya kusherehekea Siku ya Watoto duniani (uk.71). Shangwe anaimba na kucheza:

> *Kwa mateso kila siku*
> *Matayarisho yako jumbe*

*Mume wangu kama ni kodi*
*Kodi kodi kodi keshalipa*
*Msituni kujificha kila siku*
*Mvunguni kujibanza kama panya*
*Nini? Jumbe anakuja kodi*
*Mwenzenu kodi mume wangu (uk.74-75).*

Wimbo huu unaendelezwa ukurasa wa 78 na 79. Uhamasishaji kupitia ngoma ya watoto unafanya viongozi kupata ujumbe kuwa wananchi wamechoka kulipa kodi. Katibu Watemi anatuthibitishia hili anapomwambia Kada Watemi " …wakuu wameshapata habari za ngoma yako hiyo" (uk.112). Kada Watemi anamweleza Katibu Watemi:

*Kama nilivyokwambia, ilichezwa ngoma hapa, ngoma hatari kwelikweli! Ngoma ya kodi (uk.107)…lakini cha ajabu, watoto wa shule ndio manju. Wanaicheza kama wana wazimu (uk.108).*

Usemi huu unadhihirisha kuwa watoto hawa walikuwa na kipawa cha kucheza ngoma na wanaicheza kwa kuifurahia. Wanatumia kipawa chao kuhamasisha viongozi na umma kuhusu janga la kitaifa-kodi. Usemi wa Kada Watemi unatilia mkazo jambo hili. Anamwambia Katibu Watemi:

*Siyo wanataka kuwatumia. Wameshawatumia. Jana ungewaona walivyokuwa wamechemka, kama vile wamekula mirungi. Watoto wanacheza hadi wanabingirika chini. Watoto wanaimba "kama ni kodi, kodi kodi twishalipa." Wee! Hatari nakwambia (uk.109).*

**Uhamasishaji**

Kwa kurejelea tamthilia ya *Shamba ya Halaiki*, jimbo la Matengo linakabiliwa na tatizo la ujinga na upofu. Gavana Mbi anafurahia hali hii. Anasema kuwa ujinga wa Wanamatengo ndio wali wake (uk.15). Upofu wa Wanamatengo unawakilishwa kupitia Bi, Domo ambaye anamshabikia Gavana Mbi kipofu kwa kuwa anatoka katika kabila lao. Ndu'kuwili ambaye ni kiongozi wa kidini na kisiasa annamhamasisha kuhusu umuhimu wa kutupilia mbali ukabila na kukumbatia umoja:

Kuna tofauti ya kutazama na kuona. Huu si wakati wa kulaumu kabila Lile. Huu ni wakati wa kuja pamoja tusaidiane (uk.21).

Vilevile, Seneta Uma anamhamasisha Bi Domo kuhusu athari ya kuwachagua viongozi kwa msingi wa kikabila. Kiongozi huyu anasema:

*Fungueni macho muone. Ukabila utawafumba macho hadi lini? Ona majanga yanayotupata kwa kuchagua viongozi kwa msingi wa kikabila (uk.40).*

Wanamatengo wanafumbwa macho hivi kwamba wanakosa kuelewa ukweli. Hii ni kutokana na propaganda za Gavana Mbi dhidi ya Lila. Baada ya Gavana Mbi kufuja pesa za waathiriwa wa mafuriko, anampa kila Mwanamatengo shilingi mia moja na kueneza propaganda kuwa Lila ndiye aliyefuja pesa hizo. Huu si ukweli. Waathiriwa hawa kwa kukosa ufahamu wa kinachoendelea wanaandamana kumshutumu Seneta Lila. Wanaapa kumwangamiza. Sauti za kina baba zinasikika zikimshutumu Lila:

*Pesa ulipokea, Gavana Mbi katuambia,*
*Akauntiyo kazitia,*
*Gavana Mbi katusimulia,*
*Heri Gavana Mbi katusaidia, mia moja katugawia,*
*Tulidhani u mwema, kumbe watuhadaa (uk.54).*

Lila anataka kwenda kuwahamasisha wananchi na kuwaambia ukweli kuhusu tetesi hizi. Ndu'kuwili anamkanya asiende. Ndu'kuwili anaamua kwenda kuwaambia ukweli kwa niaba ya Lila (uk. 54-55). Halaiki anasema kwamba anasubiri umati wa watu ufike ili aondoe pazia (upofu) liliowafumba macho wajionee hali halisi ya mambo (uk.3). Rajua anapomwuliza vipi Wanamatengo watafaidika kutokana na mkutano huu, Halaiki anasema:

*Watazinduka. Watatambua nguvu iliyopo katika umoja. (uk.3).*

Tamthilia ya *Kifunganjia* (2021) ina changamoto mbalimbali ambazo zinazuia maendeleo kupatikana kijijini Bakunja. Kifunganjia ni neno lililo na maana ya kizuizi au kitu kinachopinga kufaulu kwa jambo fulani. Tatizo kuu linalokabili Bakunja ni uongozi mbaya. Tatizo hili limechangiwa pakubwa na upofu wa wanakijiji. Wengi wa Wanabakunja wamepofushwa hivi kwamba hawawezi kuona uongozi mbaya unaoendelezwa. Uongozi ulipitisha sheria kandamizi ambazo

zilihakikisha kuwa wananchi wa kawaida hawakaribii ghala la kijiji ili wasione uovu ambao ulikuwa ukitekelezwa na viongozi ghalani (uk.67). Wanajenga ua wa kuzunguka ghala ili mtu asione uovu ghalani. Wanaibua mikakati kandamizi ili kuwashinikiza wanakijiji kuchangia nafaka ghalani; nafaka hii wanaipora na kujifaidisha wenyewe (uk. 127).

Katika hali hii ya upofu uliokithiri Bakunja, kiongozi Rajua anajitokeza kuwahamasisha wanakijiji ili kuondoa upofu uliokuwa umewagubika. Hatua ya kwanza katika mchakato huu wa uhamasishaji ilikuwa kuondoa ua uliozingira ghala. Rajua anaondoa ua huu ili wanakijiji wajionee uovu uliokuwa ukiendelezwa na viongozi Tule na Domo ghalani (uk.1, 16). Ua ni jazanda ya upofu ambao ulikuwa umewafunika wanakijiji. Hatua hii inazaa matunda kwa kuwa wanakijiji wanapata kujionea na kuona hitaji la kuvumbua mbinu za kumaliza mchwa na panya ghalani. Ni kujionea huku ndiko kunawafanya wanakijiji kujumuika pamoja na kuchangisha hela za kuwatuma vijana maabarani kwenda kutafuta suluhu ya tatizo la panya na mchwa (uk. 3, 16, 22). Jambo hili lililenga kuondoa njaa na umaskini kijijini, hivyo kuchangia utimizwaji wa L1 na L2.

Hatua nyingine anayoutumia kiongozi Rajua kuhamasisha wanakijiji ni kuandaa mikutano ya hadhara. Katika mikutano hii, Rajua anawahutubia Wanabakunja na kuwaelimisha kuhusu umuhimu wa kutafuta suluhu ya kudumu kwa matatizo yanayokumba Bakunja. Rajua anaandaa mikutano ya kisiasa kuwahamasisha wanakijiji. Katika mikutano hii, kiongozi huyu anawaalika wageni kuja kuwafunza mama na vijana namna ya kuwaangamiza panya na mchwa (uk. 113). Isitoshe, anatumia mikutano hii kama jukwaa la kushinikiza umoja wa wakulima. Anawataka wakulima kuunda chama kimoja chenye nguvu zaidi ambacho kitawatetea (uk.113).Uhamasishaji huu unalenga kuendeleza uafikiaji wa L1 na L2. Mikutano hii ya Rajua vilevile inawakumbusha raia kuhusu haki yao kupiga kura na kuwataka kupigia kura viongozi bila kununuliwa (uk. 114). Jambo hili linaendeleza uafikiaji wa L16.

Katika tamthilia ya *Kodi*, watoto wa shule wanajitokeza kuelekeza jamii kwa kuihamasisha kupinga unyanyasaji wa kiuchumi ambao ulitishia uafikiaji wa L1. Uongozi ni shughuli ya kuwaongoza na kuwaelekeza watu kuafikia lengo fulani (Dinibutun, 2022). Hivyo basi, watoto katika *Kodi* ni viongozi. Kupitia wimbo wao: Kodi, Kodi, Kodi twishalipa, wanawahamasisha na kuwaelekeza watu kususia unyanyasaji wa kiuchumi (uk.77-79). Wanachukua hatua ya kutembea kila mtaa wakihamasisha umma. Kada Watemi anathibitisha hili:

> *Maneno waliyokuwa wanaimba mazito.*
> *Tena walikuwa wanazunguka kila mtaa*
> *(uk.109).*

Watoto wanatumia mkakati huu ili kufikia watu wengi mashinani. Mkakati huu unazaa matunda kwa kuwa wimbo huu unaenea nchini kote na kuanza kuimbwa na watu wazima (uk. 111). Wimbo wa watoto unachukuliwa kuwa wimbo wa jamii. Katika wimbo huu ujumbe unakuwa: Kodi hatulipi, kodi twishalipa (uk. 122, 130, 152).

Uhamasishaji wa wananchi katika *Kodi* unafanywa kupitia mbinu ya maandamano. Mengi ya maandamano haya yanaongozwa na vijana. Kulingana na Njoroge (2014), viongozi ni visababishi vya mabadiliko. Vijana ni viongozi wanaosababisha na kushiniza mabadiliko katika jamii ya *Kodi*. Mtambaji anathibitisha jambo hili kupitia kwa usemaji wake:

> *Toba! Toba! Lakini acha hawa wa meza, ngoma iliyo mkosha bibi ni ile ya madotcom. Yaani wao hawapigi ngoma, wala meza, wala nini, lakini angalia huo mvumo wao! (uk.128).*

Usemi huu wa Mtambaji unabainisha kuwa vijana wanatumia mbinu mpya kuendeleza maandamano yao. Mtambaji anaposema: angalia huo mvumo wao anamaanisha kuwa mbinu hizi mpya zinayafanya maandamano ya vijana kuwa na athari kubwa; athari isiyoweza kupuuzwa na viongozi. Matumizi ya teknolojia ni mojawapo ya njia zinazotumiwa kuwahamasisha vijana. Mtambaji anasema:

> *Kwani watoto hawana akili?*
> *Kwani wao kodi hawaioni?*
> *Watoto gani wanajua kodi?*
> *Watoto wa kisasa hao.*
> *Wanasoma kwenye mitandao (uk.121).*

Mbinu hii ya vijana inaleta ufanisi mkubwa kuliko matumizi ya nguvu na ngoma. Mtambaji anatuthibitishia ufanisi huu (uk.128). Maelezo ya mwandishi yanachora taswira ya namna vijana hawa walivyoyaendesha maandamano:

> *Linaingia kundi la vijana kwa maandamano, wamebeba mabango yaliyoandikwa: "Tunataka haki zetu," "Na sisi tunataka kodi zetu," kodi ni haki," wanaimba (uk.128).*

Vilevile inabainika kuwa, katika nchi hii yapo makundi ya wanaharakati ambao kazi yao ni kutetea haki kama haki ya usawa wa kijinsia (uk.37). Wanaharakati hawa ni viongozi wanaoshinikiza uafikiaji wa L5.

Kwa kurejelea tamthilia ya *Mwinyi na Manyani ya Adili* (2022), kiongozi Mwinyi anawahamasisha wananchi kuhusu maono aliyo nayo kwa nchi yake na mpango wake wa kimaendeleo ili ashirikiane nao kufanikisha ME. Anatumia vitabu kama jukwaa la kuwahamasisha wananchi. Anayaweka mawazo aliyo nayo katika vitabu. Kitabu mojawapo ni *Mzee Mwinyi na Zama za Soko Huria*. Kulingana na Mwinyi mwenyewe, kitabu hiki ni dira mpya ya kuleta mageuzi (uk.24). Njoroge (2014) kupitia utafiti wake alitambua kuwa viongozi ni vichochezi vya mabadiliko. Kupitia kitabu cha *Mzee Mwinyi na Zama za soko Huria*, Mwinyi anachochea mabadiliko kwa kuhamasisha raia kuhusu mfumo mpya wa soko huru. Kulingana naye, katika kuandika kitabu hiki, alizingatia maoni ya viongozi wa awali, viongozi waliowahi kuongoza nchi ya Tanzania (uk. 24).

Kitabu kingine alichoandika Mwinyi ni *Kila Zama na Kitabu Chake*. Anachosisitiza Mwinyi kupitia kwa kitabu hiki ni kwamba kila aina ya uongozi una mbinu na mikakati yake ya kuleta maendeleo. Jambo analomaanisha ni kuwa utawala wake utakuwa na mfumo wa soko huru au kibepari ambao ni tofauti na Mfumo wa Ujamaa yaani uongozi wake hautaendelea kuushikilia Mfumo wa Ujamaa ulioanzishwa na Rais Nyerere. Ni kupitia kitabu hiki ndipo anapowahamasisha umma kuhusu maono aliyo nayo kwa nchi yake ya Tanzania na wananchi kwa ujumla. Anasisitiza kuwa katika kipindi chake cha utawala, ana maono ya kuligeuza janga kuwa Bustani ya Edeni. Anasema:

> *Na katika miaka mitano, na kwa msaada wa Mwenyewe Mwenyezi Mungu Subhana wa Taala, mimi na serikali yangu tutaligeuza jangwa kuwa Bustani ya Edeni; Bustani ya kijani kibichi! (uk.43).*

Jangwa ni jazanda ya nchi ya Tanzania iliyokuwa imefilisika na kutamauka wakati Mwinyi alipochukua hatamu za uongozi baada ya Rais Nyerere. Bustani la Edeni ni mahali alipotaka kulielekeza taifa kupitia uongozi wake (uk. 42-43). Katika kitabu hiki anachora taswira ya Bustani ya Edeni katika Biblia kwa kuelezea aina mbalimbali ya mito iliyomo ndani ya Bustani hii kama vile Pishoni, Gihoni, Tagri na Eufrate (uk.43). Anakizindua kitabu hiki huku akishangiliwa na wananchi (uk. 47). Kwa maoni ya Ntiba (2011), viongozi wana jukumu kubwa la kuongoza raia ili waweze kupiga hatua kimaendeleo. Rais Mwinyi anajitolea kuleta maendeleo katika nchi yake. Kiongozi Mwinyi ana maono ya kukomesha umaskini na njaa nchini mwake. Hali hii itaendeleza utimizwaji wa L1 na L2.

Kitabu kingine kinachoandikwa na Rais Mwinyi na ambacho kinatumiwa kuhamasisha watu ni kitabu alichokiita: *Zama Mpya*. Kitabu hiki kinaelezea mipango aliyo nayo katika kuleta maendeleo nchini Tanzania. Anatumia kitabu hiki kama jukwaa la kuhamasisha wananchi kuhusu mipango ya kimaendeleo aliyo nayo. Mipango hii ya kimaendeleo inaendeleza uafikiaji wa MME.

Kabla ya Rais Mwinyi kuandikia na kuchapisha vitabu hivi viwili: *Mzee Mwinyi na zama za soko Huria, Kila zama na Kitabu Chake na Zama Mpya* anaandika na kuchapisha kitabu alichokiita: *Kitabu cha Zama Zile.* Katika kitabu hiki, Rais Mwinyi anaelezea Mfumo wa Ujamaa ulioanzishwa na kuendelezwa na mtangulizi wake, Rais Julius Nyerere. Anaweka wazi manufaa na madhara ya mfumo huu. Madhara ya Mfumo wa Ujamaa yalikuwa mengi (uk. 44-45). Katika kitabu hiki, Mwinyi anaeleza namna makampuni na viwanda vilivyotaifishwa (uk.45). Anasema kuwa nuru na mwangaza hauko nyuma katika enzi ya Mfumo wa Ujamaa (uk.36). Ili kutatua changamoto katika nchi yake, Rais Mwinyi anarejea katika historia ya nchi yake na kuelewa uongozi wa mtangulizi wake. Anachosisitiza mwandishi Emmanuel Mbogo ni kwamba, kabla kuanza kutambua na kutekeleza mikakati ya kutatua matatizo yanayokumba jamii fulani, viongozi wafaa waielewe historia ya jamii yao. Nadharia ya uhistoria mpya inasisitiza umuhimu wa kuelewa historia ya jamii husika. Kwa kuelewa historia ya nchi yake, Mwinyi anatambua makosa yaliyofanywa na kiongozi aliyemtangulia hivyo basi anayaepuka.

Kando na machapisho ya vitabu, Rais Ali Hassan Mwinyi anatumia falsafa kuwahamasisha wananchi kuhusu mfumo mpya wa Soko Huria. Falsafa hii anaiita *Kila Zama na Kitabu Chake*. Kwa lugha ya kiarabu: *Li –*

*Kulli ajalin kitaab* (uk. 40, 56). Kiongozi Mwinyi anawaeleza watu kuhusu falsafa hii. Anasema:

> *Falsafa yangu kuhusu maisha ni kuwa, kila kitu, kila jambo lina wakati wake. Kila zama ina kitabu chake. Li – Kulli ajalin kitab. Zama ni kiumbehai. Zama huzaliwa, zama hubadilika, zikachakaa, zikazeeka na kufa! (uk.106).*

Anachosisitisha ni kuwa, kila kipindi cha uongozi huja na changamoto, mikakati na maendeleo yake. Hivyo basi, mikakati atakayoweka ili kuleta maendeleo katika kipindi chake cha uongozi ni tofauti na aliyoiweka kiongozi mtangulizi: Mwalimu Julius Nyerere. Anaiwasilisha falsafa hii kupitia shairi (uk. 107).

Kando na falsafa, kiongozi Mwinyi anatumia kaulimbiu. Kaulimbiu ni msemo ulio rahisi ambao hutumiwa na vyama vya siasa, mashirika au kwenye matangazo ili kuhamasisha watu kufuata wazo fulani (TUKI, 2014). Kaulimbiu anayaoitumia kiongozi huyu ni Rukhsa. Rukhsa ni neno la kiarabu lenye kisawe cha Kiswahili ruhusa. Kupitia kaulimbiu hii, kiongozi wa taifa anawapa wafanyabiashara wakiwemo matajiri ruhusa ya kufanya biashara Tanzania. Kaulimbiu hii inamfanya kupewa au kujipa jina la lakabu: Mzee Rukhsa (uk.65, 73).

Hotuba ni mbinu nyingine anayotumia kiongozi Mwinyi kuwahamasisha wananchi. Hotuba hii inafanyika katika ukumbi mkubwa (uk. 38). Kupitia hotuba yake, Mwinyi anaelezea baadhi ya changamoto zilizowakumba wananchi kutokana na sera ya ujamaa (uk. 41 – 42). Isitoshe, anawaeleza watu maono aliyonayo kama kiongozi wa taifa. Anawauliza wampe miaka mitano tu na kwa miaka hiyo mitano ataleta mageuzi ya kimaendeleo nchini (uk. 43). Anatumia fursa hii vilevile kueleza mfumo wake mpya wa Soko Huria (uk. 44) na kufafanua mikakati aliyoiweka kutekeleza mfumo huu mpya (uk. 45 – 47).

Lengo la uhamasisho wa Rais Mwinyi ni kuwapa wananchi maarifa ili waweze kushirikiana na kutembea naye kuleta mabadiliko. Kama Rais huenda angeamua kuyatekeleza mageuzi au sera bila kushirikiana na wananchi. Kiongozi huijua njia na mahali anakowaelekeza wafuasi wake (Hora, 2014). Baadhi ya viongozi katika jamii halisi hufanya maamuzi muhimu bila kuwashirikisha raia. Mwinyi anaendeleza uongozi shirikishi. Aidha, lengo la pili la kuhamasisha wananchi ni kuondoa upofu na ujinga. Msuya anasema:

> *Wahafidhina wanatuita Makuwadi (wajumbe) wa nchi za magharibi. Lakini ukiwauliza kama wana tiba mbadala dhidi ya madhila, mateso, aibu, njaa, umaskini na unyonge wa Mtanzania vilivyotamalaki kote nchini! Kapa! Wanatoa macho tu! Matamko ya vinywa vyao yamejaa vigugumizi. Hayaeleweki. Akili zao fugutu, zimevamiwa na funza wa kifafa na kiharusi (uk.54).*

Inabainika kupitia usemi huu kuwa wanaopinga sera ya Rais Mwinyi wana akili fugutu yaani akili iliyopofushwa. Kunao baadhi ya watu waliopinga mfumo wa Soko Huria na kuendelea kushikilia Mfumo wa Ujamaa. Mfano wa watu hawa ni Profesa Kaduna na Dkt Sakula (uk. 48).

**Kushiriki na Kuhimiza Kilimo**

Kwa kurejelea tamthilia ya *Kodi* kunalo tatizo la njaa katika nchi (uk. 7, 8, 66). Watu wanakufa kwa njaa (uk. 31). Hali hii inatishia uafikiaji wa L2 la mpango MME. Wananchi wanachukua hatua ya kushiriki kilimo ili kuzalisha chakula. Tukiwepo na chakula cha kutosha, hali ya njaa itaondolewa. Sauti 3 anasema:

> *Mie wiki nzima kila siku, njoo kesho, njoo kesho. Nisiporudishiwa shamba langu nitalima lini na mvua zinakwisha? (uk.103).*

Mwananchi huyu anatetea umiliki wa shamba lake ili aendelee kuzalisha vyakula kupitia kilimo. Sauti 2 anamwambia sauti 1:

> *Utaacha kulima bure watoto wako wakafa njaa (uk.106).*

Usemi huu una maana kuwa wananchi, Sauti 1, 2 na 3 wakiwemo, walikuwa wakishiriki kilimo. Ndio maana wanakuja kuteta kwa Kada Watemi na Katibu Watemi ili mashamba yao yaliyokuwa yamenyakuliwa yarejeshwe. Kurejeshwa huku kungewasaidia kuondoa njaa kwani wangezalisha vyakula kupitia shughuli ya kilimo.

Kwa mujibu wa tamthilia ya *Kifunganjia*, njaa ni tatizo linaloathiri Wanakijiji wa Bakunja. Tembo anaeleza namna njaa inavyomkereza tumbo. Anamweleza Komba namna njaa imetawala nyumbani kwake hivi kwamba panya, kwa kukosa chakula, wanalazimika kula mikono yake (uk. 4). Komba anaingia nyumbani akiwa na gunia tupu. Baada ya kumkaribisha mumewe, Mama Shari anamwambia mumewe (Komba): Mbona usije basi

tulime lile shamba letu dogo la ngano? (uk.36). Kutokana na usemi wa Mama Shari, njia ya pekee kuondoa tatizo la njaa linalokumba familia yao ni kushiriki kilimo. Hata hivyo Komba hataki kujihusisha katika shughuli hii ya kiuchumi. Anachagua kukaa karibu na ghala na kwenda ulevini. Kabla ya maneno haya, Mama alikuwa ametoka shambani na kikapu ambacho mwandishi anasema kuwa hakikuwa kimejaa (uk. 34). Hii ina maana kuwa kiwango cha chakula kilichokuwa kikizalishwa Bakunja kilikuwa kimepungua kutokana na matatizo ya kiuongozi.

Ili kusuluhisha tatizo la njaa, viongozi wa awali waliwahimiza wanakijiji kujihusisha katika kilimo. Waliamua kutenga sehemu ya mazao kwenye ghala la kijiji. Hifadhi hii ya chakula ingewasaidia wanakijiji wakati wa njaa. Kuhifadhi kwa nafaka kunakuwa mkakati mojawapo wa kutatua tatizo la njaa (uk. 2, 11, 50). Katika enzi ya sasa ya uongozi wa Tule na Domo, Wanabakunja wanaamka asubuhi mapema kufanya kazi za sulubu shambani ili watokomeze njaa (uk. 1). Wanakuza vyakula mbalimbali vikiwemo ngano, miwa na mihindi (uk.8, 38, 55,128). Hata hivyo, gharama ya kukuza mimea hii inakuwa ya juu sana kwa sababu ya bei ya juu ya pembejeo (uk. 8). Uongozi wa kisiasa na kidini unawanyanyasa wakulima zaidi kwa kuwapa mikopo ghali (uk. 127). Isitoshe, viongozi hawa wanaanza kupora ghala na kufanya hifadhi ya nafaka kutokuwepo (uk. 47, 57).

Aidha, viongozi hawa wanaporomosha viwanda vya kusaga sukari kutokana na uporaji. Wakulima wanatamauka na kuanza kukata miwa yao ili kupanda mimea mingine (uk.38). Isitoshe, magugu yanavamia mashamba ya Bakunja. Uongozi unakosa mpango madhubuti wa kuyaondoa (uk.20).

Kiongozi Rajua ana maono ya kuleta maendeleo kijijini kupitia mikakati mbalimbali kilimo kikiwemo (uk. 50-52). Kwa maoni ya Mohamed (2013), uongozi mzuri ndio nguzo ya maendeleo katika jamii. Rajua ana imani kuwa kupitia kilimo maendeleo yatapatikana Bakunja: uchumi utakuzwa, umaskini utapunguzwa, uhaba wa chakula utatokomezwa, ajira ya staha kwa vijana itapatikana, matatizo ya tabia nchi yatapunguzwa na viwanda vitajengwa. Inabainika kuwa, kilimo ni mkakati muhimu wa kuafikia L1, L2, L8, L9 na L13 (uk. 15, 52-53,55,79).

**Kuanika Maovu**

Kuanika maovu ni mkakati ambao unatumiwa na viongozi ili kusaidia kufichua ukweli uliofichika, kuweka shinikizo kwa wahusika waovu wabadilike na kuwashawishi watu wachukue hatua iza kuleta mabadiliko katika jamii zao. Kwa kurejelea *Shamba la Halaiki*, iwapo maovu yaliyotekelezwa na uongozi wa Gavana Mbi yangefichwa, uongozi wake mbovu ungeendelea hivyo kuathiri uafikiaji wa MME jimboni Matengo. Mbinu moja iliyotumiwa kuanika maovu ni kupitia vyombo vya habari. Bi. Fedha anasema:

> *Kweli kabisa. Juzi waliandika habari kuhusu ziara yetu Marekani. Eti sijui tunatumia vibaya pesa za umma kujistaheresha. Mara wanapeperusha picha tukisinzia bungeni. Mara umejinunulia magari ya kifahari. Mara…(uk.30-31).*

Kulingana na muktadha huu, vyombo vya habari vinajitokeza kuanika ubadhirifu, utepetevu na ubinafsi wa wabunge.

Gavana Cheupe anasema: Maovu yao yatawekwa peupe (uk.129). Kiongozi huyu anadhamiria kuanika maovu yaliyotekelezwa na viongozi wa awali akiwemo mumewe ambaye alikuwa gavana. Katika *Kifunganjia*, Rajua anatumia vyombo vya habari kuanika maovu. Anaandika makala ambayo yanachapishwa katika gazeti la *Sauti Yetu*. Anatumia kijikamera kunasa hali halisi ghalani baada ya kuondoa ua ulioficha uovu ghalani. Kando na kunasa picha za ghala, anamhoji Mzee (uk 16). Mzee ni mwenyekiti wa baraza la wazee. Ni kupitia mahojiano haya ndipo Rajua anapata kujua historia ya ghala (uk. 18). Aidha, mikakati iliyowekwa na baraza la wazee kukabiliana na uporaji ghalani inabainishwa. (uk. 18 , 21). Mikakati hii ililenga kuangamiza tatizo la njaa hivyo kuendeleza uafikiaji wa L2.

Rajua anapoalikwa kutoa mhadhara maabarani anawapa wanafunzi nakala la gazeti la *Sauti Yetu* ili wajisomee. Baada ya kujisomea, wanafunzi wanamuuliza maswali kutokana na makala hii (uk. 48-55). Hata baada ya kuchapisha makala hii, Rajua hatulii. Anaendelea kutafuta suluhu ya kudumu. Anamweleza Shari:

> *Sifurahishwi na hali ya kijiji hiki. Hata nami nimo katika harakati ya kutafuta suluhisho. Japo sihudhurii mafunzo ya maabarani, sijakata tamaa. Upekuzi wangu kuhusu*

*maswala ya ghala umekamilika. Nimetuma makala huko Sauti Yetu lakini hilo halitoshi. Bado ninatafuta suluhisho la kudumu (uk.34).*

Usemi huu unabainisha ari, mshawasha na jitihada aliyokuwa nayo kiongozi huyu kuleta maendeleo kijijini mwake. Kwa mujibu wa Njoroge (2014), viongozi ni viasababishi vya maendeleo katika jamii. Rajua anachochewa kuwania usimamizi wa ghala ili alete maendeleo kupitia uafikiaji wa MME (uk. 80, 89).

Vyombo vya habari katika *Kodi* vinakuwa jukwaa muhimu la kuyaanika maovu katika nchi rejelewa. Vyombo hivi vinaanika kampuni hewa nchini (uk.134). Kwa kuzianika, huenda wakurugenzi wake wakachukuliwa hatua ya kisheria na vilevile wananchi wakaziambaa.

Mikakati mingine iliyobainishwa kwa kurejelea tamthilia teule ni pamoja na: kuzungumza, kupinga na kususia maamuzi mabaya; kufanya maamuzi sahihi na yenye tija kwa jamii; umoja, amani na upendo; kuwakweza na kuwabandua viongozi kupitia njia za kidemokrasia na kuhakikisha ustawi wa jamii wakati wa majanga kwa kutoa msaada wa kibinadamu.

**HITIMISHO NA MAPENDEKEZO**

**Hitimisho:** Makala hii imewasilisha matokeo na mjadala kuhusu mikakati inayotumiwa na viongozi kukabiliana na changamoto zinazokumba uafikiaji wa MME. Imebainika kuwa viongozi wanatumia mikakati mbalimbali kukabiliana na changamoto zinazokumba uafikiaji wa MME katika jamii zao. Mikakati iliyobainishwa ni pamoja na: matumizi ya elimu, taaluma, talanta na ubunifu; uhamasishaji; kushiriki na kuhimiza kilimo na kuanika maovu. Aidha, makala hii imetambua kuwa kilimo ni mkakati ambao huchangia kuafikia kwa malengo mengi ya mpango wa MME kwa mfano L1, L2, L8, L9, L13 na L15.

**Mapendekezo:** Makala hii inapendekeza kuwa mikakati inayotumiwa na viongozi kukabiliana na changamoto iwashirikishe wanaoongozwa ili kwa pamoja MME yaafikiwe. Aidha, makala hii inapendekeza kuwa, viongozi wa nchi mbalimbali waweke mikakati ya kuinua sekta ya kilimo kuanzia mashinani kwa kuwa kilimo kitasaidia kuafikia Malengo kadhaa ya mpango wa MME. Mathalani, L1, L2, L8, L13 na L15.

**MAREJELEO**


Brizee, A., & Tompkins, J. C. (2012). *New historicism, cultural studies (1980s–present)*. Purdue University.

Creswell, J. W. (2003). *Research design: Qualitative, quantitative & mixed methods approaches* (2nd ed.). Sage Publications.

Dinibutun, S. R. (2022). The effect of leadership style on organizational performance. *Journal of Management and Leadership Studies, 4*(2), 45–59. https://doi.org/10.xxxx/jmls.2022.002.00245

Greenblatt, S. (1980). *Renaissance self-fashioning: From More to Shakespeare*. University of Chicago Press.

Griggs, D., Stafford-Smith, O., Rockström, J., Öhman, M. C., Shyamsundar, P., Steffen, W., Glaser, G., Norichika, K., & Noble, I. (2013). Sustainable development goals for people and planet. *Nature, 495*(7441), 305–307. https://doi.org/10.1038/49305a

Gosling Goidsmith, J. G. (2018). *Sustainable development goals and uncertainty visualization* (Unpublished master's thesis). University of Twente.

Hora, E. A. (2014). Factors that affect women participation in leadership and decision-making position. *Asian Journal of Humanity, Art & Literature, 2*(2), 88–94.

Mbogo, E. (2022). *Mwinyi na manyani ya adili*. Africa Proper Education Network.

Mdee, J. S., Njogu, K., & Shafi, A. (2015). *Kamusi ya karne ya 21: Kamusi ya Kiswahili yenye uketo zaidi katika karne hii* (2nd ed.). Longhorn Publishers.

Mintzberg, H., Ahlstrand, B. W., & Lampel, J. (2005). *Strategy safari: A guided tour through the wilds of strategic management*. Simon and Schuster.

Mohamed, K. Y. (2013). *Masuala ya kisiasa katika ushairi wa Kandoro: Mifano kutoka katika mashairi yake* (Tasnifu ya uzamifu). Chuo Kikuu Huria cha Tanzania.

Muhando, P. (2024). *Kodi*. Mbiu Press.

Mulokozi, M. (1996). *Fasihi ya Kiswahili*. Chuo Kikuu Huria cha Tanzania.

Musindalo, M. A. (2020). *Taswira ya haki za watoto katika riwaya teule za Kiswahili za Milenia Oduori na Uteuzi wa Moyoni ya Rayya Timmamy* (Tasnifu ya uzamili). Chuo Kikuu cha Pwani.

Mwanje, J. I. (2001). *Issues in social science research: Methodology series module 1*. Organization of Social Science in Eastern & Southern Africa (OSSREA). https://www.ossrea.net/publications

Nickols, F. (2016). Strategy, tactics, and operations. *Distance Consulting LLC*. http://www.nickols.us/strategy_tactics_operations.pdf

Njoroge, A. W. (2014). *Viongozi kama visababishi vya mabadiliko katika riwaya za Mwenda Mbatiah: Vipanya vya maabara na Majira ya tufani* (Tasnifu ya uzamili). Chuo Kikuu cha Nairobi.

Ntiba, O. G. (n.d.). *Taathira ya dhamira kwa mtindo katika hadithi fupi teule za Kiswahili* (Tasnifu ya uzamili). Chuo Kikuu cha Kenyatta.

Ogonda, S. S. (2019). *Taswira ya mwanamke kiongozi katika tamthilia teule za Kiswahili* (Tasnifu ya uzamili). Chuo Kikuu cha Maseno.

Okello, D. (2016). *Shamba la halaiki*. Spotlight Publishes EA.

Okello, D. (2021). *Kifunganjia*. Story Moja Publishers.

Ongarora, S. O. (2020). *Usasa katika ushairi wa Kithaka wa Mberia: Uchanganuzi wa maudhui na mtindo* (Tasnifu ya uzamifu). Chuo Kikuu cha Nairobi.

Porter, M. E. (1996). What is strategy? *Harvard Business Review*, *74*(6), 61–78.

TUKI. (2014). *Kamusi ya Kiswahili sanifu*. Oxford University Press.

Zhai, C., Bretthauer, K., Mejia, J., & Pederaza-Martinez, A. (2023). Improving drinking water access and equity in rural sub-Saharan Africa. *Production and Operations Management*, *32*(9), 2921–2939. https://doi.org/10.1111/poms.14016